JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA

Ofisi ya Mkuu wa Polisi,
Wilaya ya Arusha,
ARUSHA.

04/01/2011

AR/B.5/VOL.II/63.

Mwenyekiti wa Chadema,
Wilaya ya Arusha,
ARUSHA.

YAH:- TAARIFA YA MAANDAMANO NA MKUTANO WA HADHARA TAREHE 5 JANUARI 2011.

Tafadhali rejea somo tajwa hao juu na barua yako yenye Kumbukumbu No. CDM/AR/W/2010 ya tarehe 31/12/2010. Kimsingi mmekubaliwa kufanya maandamano na mkutano wenu wa hadhara tarehe 5 Januari 2011, pia rejea mazungumzo yetu ya tarehe 3/1/2011 saa 12.00hrs na Kamanda wa Polisi mkoa wa Arusha ofisini kwake. Katika mazungumzo hayo tuliona kwamba kuna umuhimu wa kuchagua route moja utakayoitumia katika maandamano yenu kati ya hizi zifuatazo:-

(i) Kuanzia Phlips, Sanawari Mataa, kushuka na barabara ya AICC, Goliondoi, Sokoine Road, Friends Corner na kuingia uwanja wa NMC au

(ii) Kuanzia Philips, Sanawari mataa, Mianzini mataa, Florida Annex, Stand, CRDB Bank, Friends Corcer hadi uwanja wa NMC.

Tulifikia uamuzi huo kwa muzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Tarehe 5/1/2011 ni siku ya kazi watu wegine watakuwa wanaendelea na shughuli zao kama kawaida.
(b) Hali ya miundo mbinu ya mji wetu kwa upande wa barabara zinaeleweka zilivyo finyu, kutumia route mbili

kwa pamoja ni wazi kwamba utazuia matumizi ya barabara kwa watumiaji wengine kwa muda mrefu.

(c) Kutumia Route moja itakuwa rahisi pia kwa Jeshi la Polisi Kuandaa mpango kazi mnzuri utakaosaidia kuyaongoza Maandamano hayo vizuri na hatimaye mkutano wa hadhara.

Tafadhali naomba unipatie majibu mapema ya Route ambayo mtaitumia kati ya hizo mbili ili nami nipate muda wa kuandaa mpango kazi. Mwisho naomba washiriki katika maandamano waelimishwe kutumiza upande mmoja wa barabara na kwamba maandamano yataishia katika uwanja wa NMC kwenye mkutano wa hadhara baada ya mkutano hawataruhusiwa tena kuondoka kwa maandamano tunaomba wananchi wote watawanyike kuanzia pale uwanja wa NMC mara tu baada ya mkutano wa hadhara kumalizika.

Nawatakia maandamano na mkutano mwema utakaozingatia usalama, amani na utulivu.

Z. MWOMBEJI – SSP
MKUU WA POLSI (W) ARUSHA
ARUSHA.

MKUU WA POLISI
WILAYA YA ARUSHA

Nakaka kwa:- Kamanda wa Polisi
Mkoa wa Arusha,
ARUSHA. - Kwa taarifa tafadhali.

" " Afisa Usalama wa Taifa (W),
ARUSHA. - Kwa taarifa tafadhali

" " Katibu,
Chadema (M),
ARUSHA. - Kwa taarifa tafadhali.